

**RISALA YA WANAFUNZI WA CHUO CHA ARDHI
MOROGORO KATIKA MAHAFAJI YA 40 - TAREHE 26/11/2021**

Ndugu mgeni rasmi, ndugu wakufunzi, ndugu wageni waalikwa na ndugu wanafunzi natumai hamjambo, nawasalimu kwa jina la jamhuri ya muungano wa Tanzania.

Ndugu Mgeni Rasmi,

awali ya yote tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwako na kwa familia yako pia, kwa kukubali ombi letu la kufika apa chuoni kushiriki pamoja nasi, Ndugu mgeni rasmi tunatambua kuwa umeacha shughuri zako nyingi za kiofisi na ukakubali kuchukua muda wako kuja kujumuika nasi katika shughuli hii ya kuwaaga wenzetu kwa pamoja tunasema asante sana na Mungu akubariki na akujarie kila lililo jema akutimizie haja ya moyo wako.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Chuo chetu kinatoa kada mbili ya geomatikia (GEOMATICS) na ya mipango miji (URBAN AND REGIONAL PLANNING) katika ngazi ya astashahada na stashahada. Katika mwaka huu wa masomo, kuna jumla ya wanafunzi 501 waliosajiliwa. Kati yao, wanafunzi wa jinsia ya kiume wakiwa 346 (69%) na jinsia ya kike wakiwa 155 (31%).

Ndugu Mgeni Rasmi,

Mafanikio yaliopatikana tangu chuo chetu kianzishwe ni mengi, kwa kuyataja kwa ufupi ni kama ifuatavyo.

- ❖ Chuo kimezalisha wataalamu bora wenye weledi mkubwa katika fani ya upimaji na mipango miji
- ❖ Kusaidia kutoa elimu ya ardhi ili kuweza kutatua migogoro ya ardhi
- ❖ Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya ardhi.
- ❖ Pia chuo kimefanikiwa kuongeza darasa moja ambalo hivi sasa linajengwa ili kukabiliana na changamoto zilizokuwepo za upungufu wa vyumba vya madarasa.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Siku zote panapo mafanikio hapakosi changamoto. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto tunazokutana:

- ❖ Upungufu wa vifaa vya kujifunzia kama vile
 - Differential GPS
 - Total station
 - Computer
 - Level
- ❖ Upungufu wa miundombinu kama vile
 - Chumba cha computer kutokukidhi idadi ya wanafunzi.

- ❖ Kutokuwa na viwanja vya michezo kama vile
 - Football
 - Basketball
- ❖ Kutokuwa na bus la chuo
- ❖ Usalama mdogo kwa chuo chetu kwa kukosa uzio imara zaidi ya uliopo sasa.
- ❖ Kutokuwa na chumba cha studio kwa ajili ya wanafunzi wa mipango miji.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunakuomba kwa kushirikiana na Bodi ya chuo mzishughulikie changamoto hizo kwa manufaa mapana ya jamii ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunaomba na pia tunashauri mambo yafatayo:

- ❖ Kulingana na ongezeko la wanafunzi kila mwaka tunaomba hatua za haraka zichukuliwe ili kuhamisha chuo kulingana na ufinyu wa eneo la sasa, kwa kuendeleza eneo la Mlima Kola.
- ❖ Ndugu mgeni rasmi tunakuomba kuwepo na mfumo ambao utawawezesha wahitimu kupata ajira ili kuweza kutatua changamoto zinazo izunguka jamii kuhusiana na Ardhi.

- ❖ Ndugu mgeni rasmi tunaomba kupata vifaa ili tuweze kujifunza zaidi kwa vitendo na siyo kwa nadharia ili kupata wataalamu wabobezi wa Ardhi.
- ❖ Ndugu mgeni rasmi tunapendekeza upanuzi wa maabara ya computer na kuongezewa computer ili kuweza kutosheleza idadi ya wanafunzi waliopo.
- ❖ Ndugu mgeni rasmi tunaomba kuwekewa viti visivyo hamishika kwenye madarasa yetu.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Tunakushukuru sana kwa namna unavyoendelea kushirikiana nasi. Tunayo matumaini makubwa kwako kwamba changamoto zetu utazipatia ufumbuzi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.